








For more information visit www.livingwaters.com and click on "Save Yourself Some Pain".

# JE, WEWE NI MTU MWEMA?





UNAMWITAJE MTU ASEMAYE UONGO?
MWONGO.
JE, UMEWAHI KUIBA CHO CHOTE?
HAPANA.
LAKINI NI PUNDE TU UMENIAMBIA KUWA WEWE NI MWONGO.
AAH, NILIWAHI KUIBA PIPI MARA MOJA TU NILIPOKUWA MTOTO.
JE, MTU ANAYEIBA UNAMWITAJE?
MWIZI.
JE, UMEWAHI KUMTAZAMA MTU KWA KUMTAMANI?
NIMEWAHI.
YESU ALISEMA... "KILA MTU AMTAZAMAYE MWANAMKE KWA KUMTAMANI, AMEKWISHA KUZINI NAYE MOYONI MWAKE." (MT 5:28).
JE, UMEWAHI KULAANI KWA JINA LA MUNGU?
NAAPA KWA JINA LA... NAWEZA NIKAKU#@*#%! SAS HIVI...
HIYO NI KUFURU, "... MAANA BWANA HATAMHESABIA KUWA HANA HATIA MTU ALITAJAYE JINA LAKE BURE." (KUT 20:7)
KWA KUKIRI KWAKO MWENYEWE, WEWE NI MWONGO, MWIZI, UNA KUFURU, NA MZINZI MOYONI MWAKO. NA HIZO NI AMRI NNE TU KATI YA ZILE KUMI.
AHAA, KWAHIYO MIMI SI MKAMILIFU.
KWA KWELI HALI NI MBAYA ZAIDI...
...MAANA DHAMBI SI TU KUTENDA YALIYOKATAZWA; BALI PIA KUTOKUTENDA YALIYOAMRIWA.
"BASI YEYE AJUAYE KUTENDA MEMA, WALA HAYATENDI, KWAKE HUYO NI DHAMBI." (YAK 4:17)
YAPO ZAIDI...
INGEKUWAJE KAMA TUNGEKUWA NA KIFAA AMBACHO TUKIKIFUNGA KICHWANI KWAKO KINGEWEZA KUREKODI MAWAZO YAKO YOTE KWA MUDA WA JUMA ZIMA...
... NA HALAFU TUKAANGALIA MAWAZO HAYO KAMA VILE SINEMA MBELE YA RAFIKI ZAKO NA WANAFAMILIA YAKO.
HIYO INGEKUWA FEDHEHA!
MUNGU ANAZIJUA SIRI ZA MOYO (ZAB 44:21)
VEMA... LAKINI UKINILINGANISHA NA BAADHI YA WATU WENGINE, MIMI NAONEKANA MTAKATIFU!
7ft
KKK
NI KWELI, LAKINI KIPIMO SAHIHI NI SHERIA YA MUNGU NA WALA SI WATU WENGINE.